**BARAZA LA WAKUU WA SHULE ZA KIISLAMU TANZANIA**

**MTIHANI WA UTAMILIFU WA SHULE ZA KIISLAMU**

**KIDATO CHA PILI**

**KISWAHILI**

**MWONGOZO WA USAHIHISHAJI JULAI/AGOSTI, 2026**

Shulelibrary.com

1. Mtahiniwa kuchagua jibu lililo sahihi katika machaguo aliyopewa:

| (i) | (ii) | (iii) | (iv) | (v) | (vi) | (vii) | (viii) | (ix) | (x) |
|---|---|---|---|---|---|---|---|---|---|
| C | B | D | A | C | D | A | C | B | D |

**Alama 01 @ jibu = Alama 10**

2. Mtahiniwa anatakiwa aoanishe orodha A na orodha B.

| ORODHA A | (i) | (ii) | (iii) | (iv) | (v) |
|---|---|---|---|---|---|
| ORODHA B | E | A | G | B | D |

**Alama 01 @ jibu = Alama 05**

3. Mtahiniwa anatakiwa kutaja mambo matano yanayoathiri mazungumzo:

(i) Mada

(ii) Muktadha

(iii) Uhusiano baina ya wazungumzaji

(iv) Jinsi

(v) Umri

(vi) Lengo la mazungumzo

(vii) Shughuli iliyopo

(viii) Hali ya mzungumzaji **Alama 02 @ = Alama 10**

4. Mtahiniwa anapaswa kubainisha mambo ya kuzingatia katika kusoma kwa fasaha (mambo matano (05))

(i) Kuzingatia matamshi sahihi ya maneno

(ii) Alama za uandishi

(iii) Kasi stahiki

(iv) Mtiririko wa aya

(v) Utamkaji sahihi wa silabi zenye mkazo na kiimbo ili kupata maana sahihi.

**Alama 02 @ = Alama 10**

5. Mtahiniwa anatakiwa abainishe sifa tano za lugha ya mazungumzo:

(i) Kupeana nafasi wakati wa kuzungumza

(ii) Kutumia lugha ya mkato kwa lengo la kurahisisha mawasiliano

(iii) Kuwa na matumizi ya ishara na mijongeo ya viungo vya mwili

(iv) Kurudia neno au sentensi kwa lengo la kusisitiza

(v) Matumizi ya wazi ya mkazo na kiimbo

(vi) Matumizi ya lugha ya vionjo

(vii) Huwasilishwa kwa mdomo

(viii) Huweza kubadilika kwa haraka

**Alama 02 @ = Alama 10**

6. Mtahiniwa anatakiwa kueleza maana ya kirai na abainishe aina nne za virai:

(a) Kirai ni neno au kifungu cha maneno kinachotawaliwa na neno kuu peke yake au neno kuu na kijalizo. **Alama 02**

(b) (i) Kirai nomino (KN)

(ii) Kirai kitenzi (KT)

(iii) Kirai kivumishi (KV)

(iv) Kirai kielezi (KE)

(v) Kirai kihusishi (KH)

**Alama 02 @ = Alama 08**

7. Mtahiniwa anatakiwa kueleza kwa ufupi maana za istilahi alizopewa:

(i) Lugha ya mazungumzo – Ni lugha inayowasilishwa kwa njia ya mdomo.

(ii) Mkazo – Ni kiwango cha nguvu inayotumika katika utamkaji wa silabi katika neno.

(iii) Kiimbo – Ni kupanda na kushuka kwa mawimbi ya sauti wakati wa utamkaji.

Shulelibrary.com

(iv) Lafudhi – Ni namna ya uzungumzaji au usemaji unaoipa utambulisho jamii fulani kutokana na lugha yao ya kwanza. **Alama 2.5 @ = Alama 10**

8. Mtahiniwa anatakiwa kusoma wimbo kisha kujibu maswali ya ufahamu:

(a) Uzalendo/nchi yangu Tanzania/ Tanzania

(b) Tanzania

(c) (i) Uhuru

(ii) Amani

(iii) Uzalendo

(iv) Upendo **Alama 02 @ = Alama 10**

shulelibrary.com

9. Mtahiniwa anatakiwa abainishe aina za rejesta na mifano yake (hoja tano (5))

(a) Rejesta ya hospitalini

Mfano: Meza mbili mara tatu

(b) Rejesta ya sokoni

Mfano: Nyanya zimekufa bei

(c) Rejesta ya mgahawani

Mfano: Nani chai chapati

(d) Rejesta ya barabarani

Mfano: Konda msaada kwenye tuta

(e) Rejesta ya msikitini au kanisani

Mfano: Tumswalie Mtume

Bwana Yesu asifiwe

**Alama 01 @ x 10 = Alama 10**

10. Mtahiniwa anatakiwa aandike kumbukumbu ya mkutano wa serikali ya wanafunzi kwa ajenda tano.

MUUNDO WA KUMBUKUMBU ZA MKUTANO

(i) Kichwa cha kumbukumbu **Alama 02**

(ii) Mahudhurio

(a) Waliohudhuria (b) Wasiohudhuria (c) Maadhura (d) Waalikwa

**@00 ½ = 02**

(iii) Ajenda

- Kutaja **Alama 2 ½**
- Kuelezea **Alama 7 ½**

(iv) Saini **Alama 01**

Shulelibrary.com